ORTHODOX PATRIARCHATE OF ALEXANDRIA
Patriarch: His Beatitude the Pope and Patriarch
of Alexandria and All Africa PETROS VII.

HOLY ARCHIBISHOPRIC OF IRINOUPOLIS
His Eminence Metropolitan Makarios of
Kenya and Irinoupolis
Dean of the Seminary

Edited by:
Orthodox Patriarchal Seminary, Nairobi.

2nd edition: 2002

UTANGULIZI

Kwa kuwa, katika Seminari yetu hapa Nairobi, tunao wanafunzi kutoka nchi mbalimbali wa makabila na ukoo tofauti tofauti ambao walijitokeza kutafsiri ibada au maombi ya Kanisa la Orthodoksi katika lugha inayoeleweka na kila kabila - yaani lugha ya Kiswahili.

Jinsi vile niliwasilisha jambo hili la kutafsiri kwa hawa wanafunzi wa Seminari, wote bila shaka waliitikia na moyo wao wote. Hivi majuzi, wamejiunga katika vikundi kadha wa kadha na kuanza kazi hiyo ya kutafsiri Ibada, jambo lingine geni lilitokea - tukaonelea ya kwamba tutafsiri ibada na maombi hayo katika lugha ya kila kabila ya hawa wanafunzi. Kwa hivyo, vikundi vyao vya utafsiri vimeungana kufuatana na kabila zao. Kwa sasa, tuna ibada kadha wa kadha ambazo zimetafsiriwa kwenye lugha mbalimbali ya kila kabila. Tunatumaini ya

kuwa kazi hii itachapishwa kwa uwezo na usaidizi wa Mwenyezi Mungu.

Tunaona ya kuwa kwa kuadhimisha ibada hizi mbalimbali na kushiriki kwetu, tunapata fahamu maishani mwetu kwamba mioyo yetu huwa karibu na Roho wa Mungu. Maombi ya mara kwa mara na huduma yetu katika ibada ya Kanisa la Orthodoksi hutupa sisi tumaini la wokovu ambapo ndilo lengo letu. Maombi mazuri ya Kiorthodoksi ambayo huadhimishwa katika lugha za kimama za watu wa Mungu huleta ufanisi katika maisha yao, kuwa kama Mungu. Hivyo ni kusema kwamba hufikia kiwango cha 'theosis' - yaani kuwa kama Mungu mwenyewe.

Wanafunzi wetu wa Seminari wanatoka katika vijiji vilivyotengwa ambavyo Orthodoksi haijaenea hivi kwamba hukosa ufahamu wowote ule kuhusu Ibada za Orthodoksi zilizo nzuri na utajiri mwingi wa

Imani. Wanaposhiriki katika ibada kwenye kanisa la hapa Seminari kila mara, wao hubadilishwa na kugeuzwa kwa nje na kindani katika matendo yao.

Basi, hii ndiyo fumbo kuu ya maisha yetu katika Seminari; kwamba tunakua katika Kristo kwa kufanya maombi mara kwa mara katika kanisa letu lililo takatifu, katoliki na la mitume.

Yesu Kristo mwenyewe alituambia ya kwamba tuwe tukiomba kwake na atakuwa pamoja nasi daima.

Na Askofu Makarios wa Riruta

Kwa niaba ya Askofu Mkuu Petros Metropolitan wa Accra tena mwakilishi wa Patriaka katika Afrika ya Mashariki.

MAOMBI YA JIONI
(Vespers)

Kasisi: Ahimidiwe Mungu wetu daima, Sasa na siku zote hata milele na milele.

Watu: Amina.

Msomaji: Njoni, tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu.

Njoni, tumwinamie na tumsujudu yeye Kristo yu Mungu Mfalme wetu.

Njoni, tumwinamie na tumsujudu yeye Kristo aliye Mfalme na Mungu wetu.

Zaburi 104:

Ee Nafsi yangu, umhimidi Bwana; Wewe, Bwana Mungu wangu, Umejifanya mkuu sana; Umejivika heshima na adhama. Umejivika nuru kama vazi; Umezitandika mbingu kama pazia; Na kuziweka nguzo za orofa zake majini. Huyafanya mawingu kuwa gari lake, na kwenda juu ya mabawa ya upepo. Huwafanya malaika zake kuwa pepo. Na watumishi wake kuwa moto wa miali. Uliiweka nchi juu ya misingi yake, isitikisike milele. Uliifunika kwa vilindi kama kwa vazi, Maji yalikuwa yakisimama

juu ya milima. Kwa kukemea kwako yakakimbia, Kwa sauti ya radi yako yakaenda zake kasi, Yakapanda milima, yakatelemka mabondeni, mpaka mahali ulipoyatengenezea. Umeweka mpaka yasiupite, wala yasirudi kuifunikiza nchi. Hupeleka chemchemi katika mabonde; Zapita kati ya milima; Zamnywesha kila mnyama wa kondeni; Punda-mwitu huzima kiu yao. Kandokando hukaa ndege wa angani; Kati ya matawi hutoa sauti zao. Huinywesha milima toka orofa zake; Nchi imeshiba mazao ya kazi zako. Huyameesha majani kwa makundi, na maboga kwa matumizi ya mwanadamu; Ili atoe chakula katika nchi, Na divai imfurahishe mtu moyo wake. Aung'aze uso wake kwa mafuta, Na mkate umburudishe mtu moyo wake. Miti ya Bwana nayo imeshiba, mierezi ya Lebanoni aliyoipanda. Ndimo ndege wafanyamo vitundu vyao, Na korongo, misonobari ni nyumba yake. Milima mirefu ndiko waliko mbuzi wamwitu, na magenge ni kimbilio la mwibari. Aliufanya mwezi kwa ajili ya nyakati, jua latambua kuchwa kwake.

Wewe hufanya giza, kukawa usiku, ndipo atambaapo kila mnyama wa mwitu. Wana-simba hunguruma wakitaka mawindo, Ili kutafuta chakula chao kwa Mungu. Jua lachomoza, wanakwenda zao, na kujilaza mapangoni mwao. Mwandamu atoka kwenda zake kazini, na kwenye utumishi wake mpaka jioni. Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi matendo yako! Kwa hekima umevifanya vyote pia. Dunia imejaa mali zako.

Bahari iko kule, kubwa na upana, Ndimo mlimo viendavyo visivyohesabika, viumbe hai vidogo kwa vikubwa. Ndimo zipitamo merikebu, ndimo alimo lewiathani uliyemwumba acheze humo. Hao wote wanakungoja Wewe, uwape chakula chao kwa wakati wake. wewe huwapa, wao wanakiokota; Wewe waukunjua mkono wako, wao wanashiba mema; Wewe wauficha uso wako, wao wanafadhaika; Waiondoa pumzi yao, wanakufa, na kuyarudia mavumbi yao, waipeleka roho yako, wanaumbwa, Nawe waufanya upya uso wa nchi.

Utukufu wa Bwana na udumu milele; Bwana na ayafurahie matendo yake. Aitazama nchi, inatetemeka; aigusa milima, inatoka moshi. Nitamwimbia Bwana maadamu ninaishi; nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai; Kutafakari kwangu na kuwe kutamu kwake; mimi nitamfurahia Bwana. Wenye dhambi waangamizwe katika nchi, watendao ubaya wasiwepo tena. Ee nafsi yangu umhimidi Bwana. (Na tena) Jua latambua kuchwa kwake; Wewe hufanya giza, kukawa usiku. Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi matendo yako! Kwa hekima umevifanya vyote pia. Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, amina. Aleluya, Aleluya, Aleluya, utukufu kwako Ee Mungu x3. Ee Bwana matumaini yetu, utukufu kwako.

Wakati Msomaji anapoanza kusoma zaburi 104, Kasisi akisimama mbele ya Meza takatifu anasoma maombi haya kwa sauti ya chini.

Ombi la kwanza:

Tumwombe Bwana. Bwana hurumia.

Ee Bwana, mvumilivu, mwenye huruma nyingi na mpenda wanadamu yasikie maombi yetu na utege sikio lako kwa sauti ya dua zetu. Imarisha agano jema kwetu na utuongoze tuishi kwa ukweli wako. Furahisha mioyo yetu tulitii jina lako takatifu u mfalme wa ajabu, Mungu wa pekee hakuna Mungu mwingine, uliye Bwana wa fadhili na wa uwezo unayetusaidia, kutegemeza na kuwaokoa wanaotumaini jina lako takatifu. Kwa kuwa utukufu, heshima na usujudu ni haki yako, ya Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ombi la pili:

Tumwombe Bwana. Bwana hurumia.

Ee Bwana usitukemee na kutuadhibu kwa hasira yako, bali utupe kwa kadiri ya upendo wako uliye mganga na mponyaji wa Roho zetu. Utuongoze kwenye kimbilio la nia yako na kuangaza mioyo yetu kujua ukweli wako. Tena, utujalie usiku huu na siku zote za maisha yetu ziwe za amani

bila dhambi, kwa maombi ya mzazi Mungu mtakatifu na ya watakatifu wote; na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ombi la tatu:

Ee Bwana Mungu wa watumishi wako wenye dhambi wasiofaa, usituaibishe tutajapo jina lako takatifu na tuwekapo tumaini letu kwa rehema yako, bali utujalie kwa vyovyote vile uokovu kwa upendo wako.

Ee Bwana, utufanye wafaao kukupenda na kukuogopa kwa mioyo yetu yote na kuimarisha nia yako kwa vitu vyote. Kwa kuwa u mwenye rehema na mpenda wanadamu na kwako tunatoa utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ombi la nne:

Ee Bwana unayeadhimishwa kwa nguvu takatifu kwa nyimbo mfululizo zisizo na mwisho, ujaze vinywa vyetu na utukufu wako ili tuliinue jina lako takatifu na

utuunganishe nao wakuogopao kwa kutenda na kulinda ukweli na amri zako. Kwa maombi ya mzazi Mungu mtakatifu na watakatifu wote; na kwa kuwa utukufu wote, heshima na usujudu ni haki yako, ya Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ombi la Tano:

Ee Bwana usiye na doa, ushikaye vitu vyote mikononi mwako, mvumilivu kwetu sote unayehuzunika kwa maovu yetu. Kwa rehema, huruma na ukarimu ututazame, utujalie tuepuke usiku huu wote katika mawazo mabaya ya muovu. Uweke maisha yetu huru kutokana na shambulio lolote; kwa rehema ya roho yako yote takatifu na upendo wa mwanadamu na wa Mwana wako wa pekee mhimidiwa pamoja na utakatifu wote, mpendwa na mpaji wa uhai, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ombi la sita:

Ee Mungu wa pekee mpenda wanadamu na mfalme wa ajabu huvutaye vitu vyote

kwa upendo na amri zako kote duniani, mtawala wa vyote unayetupa ukarimu wa ufalme wako. Baraka zako nyingi tumepokea siku hii kwa kutuweka mbali na yule mwovu; utujalie tuwe bila dhambi kwa wakati uliosalia mbele ya utukufu wako takatifu tuimbe sifa zako. Kwa kuwa wewendiye Mungu wetu na kwako tunatoa utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ombi la saba:

Ee Mungu mfalme uliye mbinguni, usiyekufa, unayeishi kwa mwanga usiyofikika, uliyeumba vitu vyote kwa hekima na kugawanya mchana na usiku, ukafanya jua kutawala mchana na mwezi na nyota kutawala usiku, uliyetujalia maskini wenye dhambi kufika wakati huu, na kukaribia mbele yako kwa shukrani na kwa maombi haya ya jioni. Ee Bwana mpenda wanadamu yakiri maombi yetu yapae kwako kama uvumba na kama manukato ya kupendeza, utujalie na

kutukinga na silaha ya nuru ya kutuokoa katika hofu ya usiku na mioto ya giza na utupe usingizi imara ili tukiamuka tuwe huru bila dhambi, ndoto na fikira mbaya za shetani.

Naam, Ee Bwana mpaji wa vitu vyote vyema, tuangaze tukumbuke jina lako usiku kucha na kutafakari amri zako ili tunapoamuka tuwe na furaha ya roho na kuomba kwa ajili ya dhambi zetu na za watu wako, utazame kutoka juu na utuhurumie kwa maombi ya mzazi Mungu na kwa kuwa u mrehemiwa na mpenda wanadamu na kwako tunatoa utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu; Sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Shemasi: Kwa amani tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia *(Kyrie eleison)*
Shemasi: Kwa ajili ya amani kutoka juu na ya wokovu wa Roho zetu, tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia *(Kyrie eleison)*
Shemasi: Kwa ajili ya amani ya ulimwengu wote na kusimama imara kwa Ekklesia takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.

Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Kwa ajili ya nyumba takatifu na waingiamo kwa imani, heshima na kumcha Mungu tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Kwa ajili ya Patriaka. . . Askofu wetu mkuu (jina), makasisi waaminifu, mashemasi katika Kristo na ya wateule wote na watu; tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Kwa ajili ya Taifa letu linalo mcha Mungu, Raisi wetu na viongozi na majeshi wapendao dini, tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Kwa ajili ya mji na nchi hii, miji yote na nchi zote na waumini waishimo, tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Kwa ajili ya wasafiri nchini kavu baharini, hewani na kwa wagonjwa, wanaoteseka, mateka na kwa wokovu wao tumwombe Bwana.
Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Kwa ajili ya kuokolewa kwa kila sikitiko, ghadhabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, ee Mungu kwa neema yako.
Watu: Bwana hurumia.
Shemasi: Tumkumbuke Maria mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda wote, Bibi wetu mtukufu mzazi-Mungu na Bikira daima pamoja na watakatifu wote, hata sisi pia wenyewe kila mmoja wetu na wenzetu wote hata maisha yetu, kujiweka mikononi mwa Kristo Mungu.
Watu: Amina.

(Zaburi 141)

Ee Bwana, nimekuita, unijie hima, unijie hima, Bwana. Ee Bwana, nimekuita unijie hima; uisikie sauti ya kilio changu, uisikie sauti yangu, nikuitapo Bwana. Sala yangu ipae mbele zako kama uvumba, kuinuliwa mikono yangu kama dhabihu ya jioni; unijie hima, Bwana.

(Zaburi 142).

Uitoe nafsi yangu kifungoni, nipate kulishukuru jina lako. Wenye haki watanizunguka. Kwa kuwa wewe

unanikirimu.
(Zaburi 130)

Ee Bwana, toka vilindini nimekulilia; Bwana, uisikie sauti ya dua zangu.
Masikio yako na yaisikilize sauti ya dua zangu.
Bwana, kama wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha.
Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja; Na neno lake nimelitumainia; nafsi yangu inamngoja Bwana.
Kuliko walinzi waingojavyo asubuhi hata jioni, kama walinzi waingojavyo asubuhi, Ee Israeli umtarajie Bwana.
Maana kwa Bwana kuna fadhili, na kwake kuna ukombozi mwingi; na yeye atamkomboa Israeli na maovu yake yote.
(Zaburi 117).
Enyi mataifa yote. msifuni Bwana, enyi watu, mhimidini. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu, na uaminifu wa Bwana ni wa milele.
Na wenye haki watanizunguka, kwa kuwa wewe unanikirimu.

Utukufu kwa Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Shemasi: *(Kwa siri)*: Tumwombe Bwana.

Kasisi: *(Kwa siri)*: Jioni, asubuhi na adhuhuri twakusifu, twakuhimidi, twakushukuru na twakuomba, Ee Rabi wa wote, Bwana mpenda wanadamu. Elekeza maombi yetu mbele zako kama uvumba, na mioyo yetu isipotoshwe kwenye maneno na mafikira maovu, utuokoe kwa kila jaribio rohoni mwetu; kwa kuwa macho yetu yaelekea kwako ewe Bwana na tumekukimbilia wewe, usituaibishe, Ee Mungu wetu. *(Kwa sauti)* Kwa kuwa utukufu wote na heshima na usujudu ni haki yako, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele.

Watu: Amina.

Shemasi: *(Kwa mnong'ono)* Rabi, bariki kuingia kutakatifu.

Kasisi: *(Kwa mnong'ono)* Kubarikiwe kuingia kwa watakatifu wako, daima; sasa na siku zote hata milele na milele.

Shemasi: *(Kwa mnong'ono)* Amina.

(Kwa sauti) Hekima! Simameni wima. We nuru ya furaha ya utukufu mtakatifu, ya Baba asiyekufa, wa mbinguni, mtakatifu, mhimidiwa, Yesu Kristo! tukiwa tumefika wakati wa kuchwa kwa jua na kuona mwanga wa jioni twamwimbia Baba, Mwana na Roho Mtakatifu Mungu. Ni wajibu wakati wote usifiwe kwa sauti safi, Ee Mwana wa Mungu, mpaji wa uhai; kwa hivyo dunia yakutukuza.

Shemasi: Jioni prokimeno.

Jamatatu:

(Zab. 4:3b) Bwana atanisikia nimwitapo.

Msomaji: Umesikia maombi yangu wakati nikuliliapo, ee Bwana wa haki yangu!

Msomaji: Bwana atanisikia nimwitapo.

Jumanne:

(Zab. 23: 6a) Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu.

Msomaji: Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu.

Msomaji: Wema na fadhili zitanifuata, siku zote za maisha yangu.

Jumatano:

(Zab. 54:1) Ee Mungu, kwa jina lako

uniokoe, na kwa uweza wako unifanyie hukumu.

Msomaji: Sikiliza ombi langu, Ee Bwana na ukubali kilio changu.

Msomaji: Ee Mungu kwa jina lako uniokoe, na kwa uweza wako unifanyie hukumu.

Alhamisi:

(Zab. 121:2) Msaada wangu u katika Bwana aliyezifanya mbingu na nchi.

Msomaji: Nitainua macho yangu kutoka milimani ambapo msaada wangu watoka.

Msomaji: Msaada wangu u katika Bwana, aliyezifanya mbingu na nchi.

Ijuma:

(Zab. 59: 9b - 10a) Mungu ndiye aliye ngome yangu, fadhili zangu atazitangulia.

Msomaji: Ee Mungu, unitoe kwa adui wangu, na uniokoe kwa wale wanaoshindana nami.

Msomaji: Mungu ndiye aliye ngome yangu, fadhili zangu atazitangulia.

Jumamosi:

(Zab. 93:1) Bwana ametamalaki, amejivika adhama.

Msomaji: Bwana amjivika, Bwana amejifunga na kujikaza nguvu.

Msomaji: Kwa kuwa amekaza nchi, ili isitikisike.

Jumamosi / Jumapili:

(Zab. 134:1) Tazama, enyi watumishi wa Bwana, mhimidini Bwana, nyote pia.

Msomaji: Wewe usimamaye katika Nyumba ya Bwana tena katika chumba cha Mungu.

Msomaji: Tazama, enyi watumishi wa Bwana, mhimidini Bwana, nyote pia.

Shemasi: Tuseme sisi sote kwa roho zetu na kwa mawazo yetu yote, tuseme hivi.

Watu: Bwana hurumia *(Kyrie eleison)* x 3.

Shemasi: Ee Bwana mwenyezi Mungu wa mababa zetu, tunakuomba utusikilize na kutuhurumia.

Watu: Bwana hurumia x 3.

Shemasi: Utuhurumie Ee Mungu Kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba utusikilize na kutuhurumia.

Watu: Bwana hurumia x 3.

Shemasi: Tena tunakuomba kwa ajili ya Patriaka wetu.... Askofu wetu mkuu (jina)

Watu: Bwana hurumia x 3.

Shemasi: Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, makasisi, mashemasi, watawa na

ndugu wetu wote katika Kristo.

Watu: Bwana hurumia x 3.

Shemasi: Tena tunakuomba kwa ajili ya watumwa wa Mungu, wakristo wote wa Orthodoksi watawa, wanaokaa au kupita katika mji huu na parishi hii, washirika, wasimamizi, wanaoweka wakfu katika nyumba hii takatifu; ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, msaada na maondoleo ya dhambi.

Watu: Bwana hurumia x 3.

Shemasi: Tena tunakuomba kwa ajili ya warehemiwa wajengaji wa nyumba hii takatifu, ambao ni kwa makumbusho heri hata ya Baba na ndugu zetu zote wa Orthodoksi warehemiwa, ambao wamelala hapa na mahali popote.

Watu: Bwana hurumia x 3.

Shemasi: Tena tunakuomba kwa ajili yao wanaotenda matendo mema katika nyumba hii takatifu na heshimiwa, kwa ajili yao wenye juhudi, wanaoimba, hata ya watu wote wanaosimama hapa, wakingoja huruma yako kubwa na utajiri.

Watu: Bwana hurumia x 3.

Kasisi: Kwa kuwa u Mungu mwenye huruma na mpenda wanadamu; na kwako tuna utoa utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, Sasa na siku zote hata milele na milele.

Watu: Amina.

Msomaji: Ee Bwana utujalie, jioni hii tusiwe na dhambi. Wahimidiwa, Ee Bwana Mungu wa Baba zetu na jina lako limesifiwa na limetukuzwa milele, Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, tunavyokutumaini wewe. Wahimidiwa, Ee Bwana unifundishe zilizo haki zako. Wahimidiwa; Ee Rabi; unifahamishe zilizo haki zako. Wahimidiwa Ee Mtakatifu; uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana, huruma yako ni ya milele; usidharau viumbe vya mikono yako. Sifa ni zako, kukuimbia ni kwako na utukufu ni wako, wa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Shemasi: Tumalize maombi yetu ya jioni kwa Bwana.

Watu: Bwana hurumia.

Shemasi: Utusaidie, utuokoe, utuhurumie,

utuhifadhi ee Mungu kwa neema yako.

Watu: Bwana hurumia.

Shemasi: Jioni hii yote iwe kamili, takatifu, tulivu na bila dhambi, tuombe kwa Bwana.

Watu: Kidhi, ee Bwana.

Shemasi: Kwa ajili ya malaika wa amani, mwongozi mwaminifu, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

Watu: Kidhi, Ee Bwana.

Shemasi: Kwa ajili ya msaada na maondoleo ya dhambi na makosa yetu, tuombe kwa Bwana.

Watu: Kidhi, Ee Bwana.

Shemasi: Kwa ajili ya vitu vyema vifaavyo kwa roho zetu na amani ya ulimwengu wote, tuombe kwa Bwana.

Watu: Kidhi, Ee Bwana.

Shemasi: Kwa ajili ya kumaliza maisha yetu yanayobaki kwa amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Watu: Kidhi, Ee Bwana.

Shemasi: Tuombe ili mwisho wa maisha yetu yawe ya kikristo kwa amani, bila maumivu, aibu, tena tuone teto njema mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

Watu: Kidhi, Ee Bwana.

Shemasi: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda wote, Bibi wetu mtukufu mzazi-Mungu na bikira daima, pamoja na watakatifu wote, hata sisi pia wenyewe na kila moja wetu na wenzetu wote, hata maisha yetu, tujiweke mikononi mwa Kristo Mungu.

Watu: Kwako, Ee Bwana.

Kasisi: Kwa kuwa u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na kwako tunatoa utukufu, kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele.

Watu: Amina.

Kasisi: Amani kwa wote.

Watu: Na iwe kwa roho yako.

Shemasi: Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

Watu: Kwako, Ee Bwana.

Kasisi: *(Kwa mnong'ono)* Ee Bwana Mungu wetu, uliyeleta mbingu karibu nasi na kuja duniani kwa wokovu wa wanadamu; tazama watumishi wako wanaoinamisha vichwa na shingo zao kwako, uliye Mungu

wa kuogopeshwa na hakimu mpenda wanadamu, wakiwa hawatumaini msaada kutoka kwa mtu, lakini hutegemea huruma yako tu na hutazama wokovu wako. Uwalinde wakati wote tena katika jioni hii usiku ujao washinde maadui wao, kutoka kwa vitendo vyo vyote vya mwovu, mawazo ya siyo faa na ufahamu uovu.

(kwa sauti): U himidiwe na utukuzwe ufalme wako, wa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, Sasa na siku zote hata milele na milele

Watu: Amina.

Apostica za jioni:

Mstari 1: (Zab. 123: 1 - 2) Nimekuinulia macho yangu, Wewe uketiye mbinguni. Kama vile macho ya watumishi kwa mjakazi kwa mkono wa Bwana zao; kama macho ya mjakazi kwa bibi yake; hivyo macho yetu humwelekea Bwana, Mungu wetu, hata atakapoturehemu.

Mstari 2: (Zab. 123: 3 - 4)

Uturehemu, Ee Bwana uturehemu sisi. kwa maana tumeshiba dharau. Nafsi zetu zimeshiba mzaha wa wenye raha, na

dharau ya wenye kiburi.

(Jumamosi) - Mstari 1: (Zab. 93:1)

Bwana ametamalaki, amejivika adhama; Bwana amejivika, na kujikaza nguvu.

Mstari 2: (Zab. 93: 2)

Naam, ulimwengu umethibitika usitikisike.

Mstari 3: (Zab. 93: 5)

Utakatifu ndio uifaao nyumba yako, Ee Bwana, milele na milele.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Sasa, Bwana umruhusu mtumishi wako kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, ulioweka tayari machoni pa watu wote; Nuru ya kuwa mwangaza wa mataifa na kuwa utukufu wa watu wako Israeli. (Luka 2: 29 - 32)

Msomaji: Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Msiyekufa Mtakatifu utuhurumie x 3.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Ee Utatu mtakatifu kamili, utuhurumie, Bwana utusamehe dhambi zetu Rabi utuondolee makosa yetu, Mtakatifu utukarimbie na kutuponya ugonjwa wetu, kwa ajili ya jina lako.

Bwana hurumia x 3.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, Sasa na siku zote hata milele na milele, Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kila siku. Na utusamehe deni zetu, kama nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Tena usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.

Kasisi: Kwa kuwa ufalme na nguvu na utukufu ni wako, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele.

Watu: Amina.

(apolytikia / Nyimbo)

Shemasi: Hekima.

Kasisi: Ahimidiwe Kristo Mungu wetu daima sasa na siku zote hata milele na milele.

Watu: Amina.

Msomaji: Uimarishe Ee Bwana imani takatifu ya wakristo wa Orthodoksi, pamoja na Ekklisia yake takatifu na mji huu hata milele na milele, Amina.

Bwana hurumia x 3. Ee Rabi mtakatifu bariki.

Kasisi: Utukufu kwako, Ee Kristo Mungu wetu, matumaini yetu, utukufu kwako.

(Ikiwa ni Jumamosi, anzia kwa:-),

Uliyefufuka Kristo Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya mama yake asiye na doa, mtakatifu kamili kwa nguvu ya msalaba wenye thamani na mpaji wa uhai; kwa ulinzi wa malaika waheshimiwa wa mbinguni; kwa maombi ya Yohana, Nabii mtangulizi na mbatizaji, mheshimiwa na wa sifa; ya Mitume watakatifu, watukufu na wasifiwa; ya Mashahidi watakatifu, waheshimiwa na washindaji wazuri; ya watawa watakatifu na wenye haki ya (Mtakatifu wa siku) tunayekumbuka leo, na ya watakatifu wote; utuhurumie na utuokoe, Ee Mungu mwema mrahimu na mpenda wanadamu.

Kwa maombi ya mababu wetu watakatifu ee Bwana Yesu Kristo Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

Watu: Amina.